

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA NJOMBE**



Novemba 03,2022

TAARIFA KWA UMMA

Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe Bi. Judica Omari leo Novemba 03, 2022 ameongoza kikao kazi cha kupitia taarifa za robo ya kwanza 2022/2023 kilichofanyikia katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Katika kikao hicho wamehudhulia Wakurugenzi Watendaji wote wa Halmashauri za Mkoa wa Njombe wakikaribishwa na Mkurugenzi mwenyeji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratus akiwakilishwa na Bw. Gilbert Ngailo.

Pamoja na mambo mengine Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe Bi. Judica Omari amewapongeza Wakurugenzi wote kwa ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani na kuwasihhi kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo lililowekwa kwa mkoa mzima wa Njombe.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

**Chrispin B. Kalinga
Kaimu Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Mkoa wa Njombe**